

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA KIWANDA KIDOGO CHA KIKUNDI CHA  
USEREMALA MKONGONI IKWIRIRI KWA KIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE  
WA UHURU MWAKA 2017.**

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa, Ndugu **Amour Hamad Amour**; Karibu sana Ikwiriri wewe pamoja na msafara wako.

Mbele yako ni Kikundi cha Useremala cha vijana Mkongoni ambao tumejiunga kwa pamoja ili kuunganisha nguvu zetu kwa kuongeza mtaji pamoja na kujiongezea kipato.

Ndugu kiongozi wa mbio za Mwenge Mradi huu umeanza tarehe 01/01/2000 ukiwa na wanachama waanzilishi 40, mpaka sasa kikundi kina wanachama 48 na wanaojifunza 18. Kikundi chetu kina akaunti **Na. 21310007107 KIKUNDI CHA MKONGONI NMB** Kibiti.

Mradi huu una thamani ya Jumla ya Tsh **20,000,000.00** ikiwa ni nguvu zetu sisi wenyewe.

Aidha tunapenda kuishukuru Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kwa kuwa tumekuwa na ushirikiano mzuri na wamekuwa pamoja nasi kwa kutupa ushauri na hata kutuwezesha kwa njia ya mkopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambapo kwa mwaka 2015/2016 tuliweza kupata mkopo wa Tsh 2,000,000.00 na tumewezeshwa kupata kazi ya kutengeneza madawati yapatayo 50 yenye thamamani ya Tsh 8,250,000.00. Madawati haya hatujayakamilisha na pia mkopo hatujarejesha kutokana na Serikali kusimamisha shughuli za uzalishaji wa bidhaa za misitu kwa zaidi ya miezi sita kuanzia Septemba 2016 hadi Februari 2017. Kwa kuwa sasa zuio hilo limeondolewa, tumajipanga kumaliza *“order”* za wateja, kulipa mikopo na kumalizia kazi ya kutengeneza madawati ya Halmashauri kabla ya Julai 2017.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge, Kikundi na jamii kwa ujumla kimenufaika na ajira kwa vijana, vijana kupata mafunzo na kupunguza ukaaji wa kwenye vijiwe ambapo tungeathirika na uzururaji na matumizi ya madawa ya kulevyaa.

Tunaiomba Serikali iendelee kutuwezesha mikopo yenye riba nafuu ili tuweze kuboresha maisha yetu na kulipa ushuru na kodi.

Ndugu kiongozi wa Mbio za Mwenge, kwa heshima na taadhima tunakuomba ukague mradi wetu.

*“Mwenge Oyee”*

**“UWEZESHAJI WA VIJANA OYEE”**

**ATHUMANI YUSUF MSANGU**

**KATIBU MSAIDIZI WA KIKUNDI**